



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BENKI KUU YA TANZANIA**



**21 Novemba 2024**

**TAARIFA KWA UMMA**

**ORODHA YA MAJUKWAA NA PROGRAMU TUMIZI “APPLICATIONS”  
ZILIZOFUNGIWA KUJIHUSISHA NA UTOAJI WA MIKOPO KIDIJITALI**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha Umma kuwa imebaini kuwepo kwa Majukwaa na Programu Tumizi ‘Applications’ zinazojihusisha na utoaji wa mikopo kidijitali bila ya kuwa na leseni na idhini kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Majukwaa na Programu hizo zimeshindwa kukidhi matakwa ya Mwongozo kwa Watoa Huduma Ndogo za Fedha wa Daraja la Pili wanaotoa huduma za mikopo kwa njia ya kidijitali wa mwaka 2024 uliotolewa na Benki Kuu tarehe 27 Agosti, 2024 (*Guidance Note on Digital Lenders Under Tier 2 Microfinance Service Providers, 2024*).

Mwongozo huo unalenga kuimarisha usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha Daraja la Pili nchini na kuhakikisha uzingatiwaji wa Kanuni za Kumlinda Mlaji wa Huduma za Fedha, ikijumuisha uwazi, uwekaji wa tozo na riba, njia za ukusanyaji wa madeni, na utunzaji wa taarifa binafsi za wateja na kulinda faragha zao.

Kupitia taarifa hii, Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuarifu Umma kwamba Majukwaa na Programu Tumizi “Applications” zifuatazo hazina kibali na haziruhusiwi kuendelea na shughuli za utoaji mikopo kidijitali;

1. BoBa Cash	19. Hewa Mkopo	37. Money Tap	55. Soko loan
2. Bolla Kash - Bolla Kash Financial Credit	20. Hi Cash	38. Mpasso chap loan - Mkopo kisasa	56. Sunloan
3. BongoPesa-Personal Online Loan	21. HiPesa	39. Mum loan	57. Sunny Loan
4. Cash Mkopo	22. Jokate Foundation Imarisha Maisha	40. My credit	58. Swift Fund
5. Cash pesa	23. KOPAHAPA	41. Nikopeshe App	59. TALA
6. Cash poa	24. Kwanza loan	42. Nufaika Loans	60. TikCash
7. CashMama	25. L-Pesa Microfinance	43. Okoa Maisha - Mkopofast	61. Twiga Loan

8. CashX	26. Land cash	44. Pesa M	62. TZcash
9. Credit Land	27. Loanplus	45. Pesa Rahisi	63. Umoja
10. Eaglecash TZ	28. M-Safi	46. PesaPlus	64. Usalama Na Uwakika Mkopo Dk15
11. Fast Mkopo	29. Mkopo Express	47. PesaX	65. Ustawi loan
12. Flower loan	30. Mkopo Extra	48. Pocket loan	66. Viva Mikopo Limited
13. FUN LOAN	31. Mkopo haraka	49. Pop Pesa	67. VunaPesa
14. Fundflex	32. MkopoFasta	50. Premier loan	68. Yes Pesa
15. Get cash	33. MkopoHaraka	51. Safe pesa	69. ZimaCash
16. Getloan	34. Mkopohuru	52. SasaMkopo	
17. Getpesa Tanzania	35. Mkoponafuu	53. Silk loan	
18. Hakika loan	36. Mkopowako	54. Silkda Credit	

Benki Kuu inautahadharisha Umma kutojihusisha na Majukwaa na Programu Tumizi “Applications” hizo. Aidha, Benki Kuu inashirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuzifungia programu hizi ili kuepusha Umma kutumia huduma za fedha zisizokuwa na vibali vya Mamlaka husika.

Benki Kuu imechapisha na itaendelea kuhuisha orodha ya watoa huduma walioidhinishwa kutoa huduma za mikopo katika tovuti yake.

Taarifa hii inapatikana kupitia tovuti ya Benki Kuu: <https://www.bot.go.tz/Other/Orodha%20ya%20Watoa%20Huduma%20Ndogo%20za%20Fedha%20wa%20Daraja%20la%20Pili.pdf>

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na: Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, S.L.P 2939, 11884 Dar es Salaam, Simu Na. +255 22 223 5586; Barua Pepe: [info@bot.go.tz](mailto:info@bot.go.tz)

**Emmanuel M. Tutuba**

**GAVANA**